# DONDOO MUHIMU ZA SHERIA YA FEDHA 2022

Dondoo muhimu za Uchambuzi wa Sheria ya Fedha 2022.

Tarehe 30 Juni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliupitisha mswaada wa fedha ambao ulisainiwa kuwa sheria na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe Samia Suluhu Hassan tarehe Mosi Julai 2022. Mswaada huu unafanya marekebisho ya jumla ya sheria 37.

01

## Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania Sura ya 197

- Kiwango cha ukomo wa serikali kukopa kutoka benki kuu sasa kutozidi 18% ya kiwango cha bajeti ya mapato ya ndani ya serikali tofauti na awali. Marekebisho haya yanaweza sababisha ongezeko la deni la taifa kutokana na ongezeko hili.

02

## Sheria ya Usajili wa Majina ya Biashara Sura ya 213

- Tafasri ya neno mmiliki mnufaika(Beneficial Owner) sasa kuendana na ile iliyorekebishwa kwenye Sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423.
- Orodha ya wamiliki wanufaika inaweza kuhitajika na mamlaka za kiuchunguzi kama vile TAKUKURU, Kitengo cha kudhibiti fedha haramu na mamlaka nyinginezo zenye mamlaka ya kiuchunguzi. Mabadiliko haya yanalenga kuongeza ufanisi na kuzuia uwezekano wa utakatishaji wa fedha kwenye biashara zinazoendeshwa kwa mifumo ya ubia tofauti na awali ambapo biashara zinazoendeshwa kwa ubia hazikuwa na takwa na kuwasilisha taarifa za wamiliki wanufaika.
- Wadau wote wa biashara za ubia(Partners) ikiwemo mawakili sasa kuwasilisha taarifa za wamiliki wanufaika wakati wa usajili kwa biashara zinazoendeshwa kwa ubia kwa msajili wa biashara.
- Wamiliki wa biashara za ubia wataokashindwa kuwasilisha taarifa za wamiliki wanufaika kwa msajili kupigwa faini isiyopungua shillingi million moja(1) na isiyozidi shillingi million tano(5)

03

## Sheria ya Tasnia ya Korosho Sura ya 203

Mgawanyo wa mapato yatokanayo na korosho, 50% ya mapato kupelekwa kwenye mfuko mkuu wa hazina na 50% kupelekwa wizara ya kilimo tofauti na awali ambapo mapato yote yalipelekwa mfuko mkuu wa hazina. Mabadiliko haya yanaweza pelekea kudolola kwa zao kwa korosho.

04

## Sheria ya Makampuni Sura ya 2012

Tafasri ya neno mmilki mnufaika imerekebishwa ili kuendana na ile ya kwenye sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu.

Sheria inaweka takwa la lazima kwa wafilisi( Liquadators) wa makampuni kutunza kumbukumbu za hesabu na nyaraka zinazohusiana na ufilisi wa makampuni angalau kwa miaka kumi tangu kuanza kwa tarehe ya kufilisiwa kwa kampuni husika.

Makampuni ambayo au afisa ambayo yatashindwa kutunza rejesta ya wanachama na wamiliki wanufaika au kutoa taarifa ya mabadiliko kwenye rejesta, kushindwa kuweka fahirisi ya majina ya wanachama na wamiliki wanufaika wa kampuni, kupigiwa penati  ya shillingi laki moja na isiyozidi million moja.

# 05 Sheria ya Hakimiliki na Hakishirikishi Sura ya 218

- Sheria inafuta COSOTA na kuanzisha ofisi itakayoshughulika na hatimiliki, maslahi na haki za wasanii.

- Taasisi za usimamizi jumuishi(Collective Management of Copyright) kuanzishwa ambazo pamoja na mambo mengine zitakuwa na majukumu ya kusisitiza ubunifu katika sekta ya Sanaa, kutoa elimu ya umuhimu wa hatimiliki kwa umma Pamoja na mambo mengine yanayofanana na hayo. Mabadiliko haya yanalenga kuongeza ufanisi na kupunguza malalamiko ya mda mrefu ya wadau wa Sanaa.

- Taasisi yoyote au mtu yoyote itakayofanya kazi kama taasisi ya usimamizi jumuishi itakayofanya kazi hapa nchini bila kibali itakuwa/amekuwa kosa la jinai na itapigwa faini isiyopungua million kumi(10) na isiyozidi million ishirini( 20).

- Watumishi wa bodi au ofisi ya hatimiliki kutochukuliwa hatua zozote za kisheria kwa masuala watakayoyafanya wakati wakitekeleza majukumu yako ya kikazi.

- Mtu huyo kama atakuwa hajaridhika na maamuzi ya ofisi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwa Waziri mwenye dhamana ya Sanaa.

- Sasa kutakuwa na tozo ya 1.5% katika vifaa vinavyotumika kuzalisha, kusambaza, kudurufu, na kutunza kazi za Sanaa, uandishi na ubunifu mwingine.

- Hakuna taasisi ya usimamizi jumuishi itakayofanya kazi Tanzania isipokuwa kama itakuwa imesajiliwa na kupewa leseni na ofisi ya usimamizi wa hatimiliki.

- Hakuna taasisi itasajiliwa kama taasisi ya usimamizi jumuishi kama kuna taasisi ya namna hiyo imesajiliwa tayari.

- Taasisi zote za usimamizi jumuishi ambazo zitakuwa zimesajiliwa hapa nchini zitalazimika kuwasilisha taarifa zao za mwaka za mapato na matumizi zilizokaguliwa pamoja na taarifa zao za utendaji kazi kwa mwaka kwa mujibu wa sheria ya Makampuni na sheria zinazofanana na hizo.

- Mtu yeyote ambae hatoridhika na maamuzi ya taasisi ya usimamizi jumuishi atakuwa na haki ya kukata rufaa kwenye ofisi ya usimamizi wa hatimiliki

06

## Sheria ya Mawasiliano ya Kielectronic na Posta Sura ya 306

Kimeongezwa kifungu kipya cha 164B ili kutoza ada ya matumizi ya king"amuzi kulingana na kiwango cha matumizi ambapo mtumiaji atali-pa kiasi cha shilingi 500 mpaka 2000.

Waziri wa mawasiliano kwa kushirikiana na Waziri wa fedha atatunga kanuni kuweka utaratibu wa namna gani tozo hizi zitatozwa. Mabadiliko haya yanaweza kupelekea watan-zania wenye uwezo wa chini kushindwa kumudu gharama za vifurushi.

07

## Sheria ya Bima Sura ya 294

Wamiliki wote wa majengo ya biashara, masoko ya umma, bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, vyombo vya majini na vivuko kuwa na bima kama takwa la lazima.

Waziri atatunga kanuni kuainisha ni aina gani ya majengo ya kibiashara, masoko ya umma na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi ambazo zitahitaji kuwa na bima kama takwa la lazima.

08

## Sheria ya Ardhi Sura ya 113

Mda wa kulipa riba ya kodi ya pango ya ardhi sasa kuwa miezi 12 tofauti na ile ya awali ambayo ilikuwa miezi sita(6). Mabadiliko haya yatatoa fursa kwa watanzania wote kulipa riba hiyo.

# 09 Sheria ya Michezo ya Kubahatisha Sura ya 41

Tafsiri ya neno ushindi imerekebishwa na sasa itajumuisha kupokea kiwango cha fedha au malipo ikiwemo zawadi, tuzo ambayo itatolewa kwa mfumo wa fedha, vito vya thamani, au mali yoyote baada ya mtu kuwa ameshiriki katika mchezo wa kubahatisha kwa mujibu wa Sheria ya Michezo ya Kubahatisha. Mabadiliko haya yanalenga kutanua wigo wa ukusanyaji wa mapato yatokanayo na michezo ya kubahatisha tofauti na awali ambapo tafsiri ya neno hili ilikuwa haijumuishi upokeaji wa zawadi au vito vya thamani.

Tafsiri ya neno wakala wa kuzuia kodi itokanayo na michezo ya kubahatisha(Withholding agent) imerekebishwa ambayo sasa itasomeka “mtu yeyote mwenye wajibu wa kuzuia kodi itokanayo na michezo ya kubahatisha baada ya mtu kushinda kwa mujibu wa Sheria ya Michezo ya Kubahatisha na kuwasilisha kiwango alichozuia kwa kamishina wa kodi nchini. Mabadiliko haya yanatoa takwa kwa makampuni yanayoendesha michezo ya kubahatisha kumkabidhi mshindhi fedha ambayo tayari inajumuisha kodi zote kwa mujibu wa sheria.

Masharti yote yaliyomo katika Sheria ya Utawala wa Kodi( The Tax Administration Act) ikiwemo utoaji wa rist za EFD, utunzaji wa nyaraka, madeni ya kodi, madai ya kodi, riba za kikodi, mapingamizi ya kikodi, rufaa za kikodi yatatumika katika katika kodi zitokanazo na michezo ya kubahatisha kwa mujibu wa Sheria ya Michezo ya Kubahatisha.

Casino zote za ardhini zitatozwa kodi kwa kiwango cha 12% ya thamani ya fedha aliyoshinda mshindi.

Michezo yote ya kubahatisha itatozwa kodi kwa kiwango cha 10% ya kiwango cha fedha alichoshinda mshindi.

Kamishina wa kodi anaweza kuweka miongozo ya namna kodi hiyo itakusanywa na kuwawasilishwa.

Makampuni yote yanayoendesha michezo ya kubahatisha yatakuwa wakala wa kukata au kuzuia kodi kabla ya mshindi hajakabidhiwa fedha zake, na kwahiyo basi, makampuni hayo yatakuwa na wajibu wa, kukabidhi fedha kwa mshindi huku kiwango hicho kikiwa kimekatwa kodi kwa mujibu wa sheria, kuwasilisha kiwango cha kodi kilichozuiwa kwa kamishina wa kodi siku saba(7) za mwezi ambao malipo yalifanyika, kuwasilisha ritani au cheti cha uthibitisho kwamba kodi imewasilishwa kwa kamishina siku 15 kabla ya mwaka wa kalenda ya serikali ya kila mwaka haujafika kikomo.

Kampuni zenye leseni ya kuendesha michezo ya kubahatisha au wakala wa kuzuia kodi itokanayo na mapato ya michezo ya kubahatisha ambazo hazitowasilisha kodi kama ilivyoanishwa katika sheria hii zitatakiwa kulipa kiasi chote cha fedha ambacho hakikuwasilishwa kikiambatana na riba Pamoja na penati kama zilivyoanishwa katika Sheria ya Utawala wa Kodi.

## 10 Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332

Tafsiri ya neno biashara sasa kujumuisha vyanzo vya mapato ya biashara za mtandaoni, kielektroniki, intanet ikiwemo miamala itakayofanyika kwa njia ya mtandao(digital market place) bila kujali namna biashara hiyo itakavyofanyika tofauti na awali ambapo neno biashara lilijumuisha mapato yatokanayo na ajira, uwekezaji na faida ya biashara ambayo kwa mwaka haizidi shillingi million nne(4).

Tafsiri mpya ya neno digital market place ikiwa na maana ya jukwaa linalowezesha kufanyika kwa muamala wa moja kwa moja kati ya muuzaji na mununuaji kupitia mtandao.

Raia wote wa kigeni watakaopokea muamala kutoka kwa mtu unaotokana na mapato kutoka Tanzania isipokuwa miamala inayotokana na biashara, kwa huduma iliyotolewa kupitia njia ya kielektroniki atalipa kodi ya mapato kwa malipo yaliyopokelewa ndani ya

Waziri wa fedha kuwa na mamlaka ya kusamehe kodi ya mapato kwa uwekezaji chini ya sheria ya uwekezaji sura ya 38 baada ya kupata ridhaa kutoka baraza la mawaziri.

Raia hao wa kigeni watakuwa na wajibu wa kuwasilisha ritani kwa kamishina wa kodi baada au kabla ya siku saba(7) ya mwezi au ndani ya mwezi ambao kodi hiyo inahusiana.

## 11 Sheria ya mamlaka za miji midogo na halmashauri za wilaya Sura ya 287 na Sheria ya Mamlaka za manispaa na majiji Sura ya 288

Mamlaka zote za miji midogo na halmashauri za wilaya Pamoja na mamlaka zote za manispaa na majiji kuwa vituo vya Pamoja vya kuratibu, kuwezesha na kusaidia mazingira bora ya ufanyaji biashara katika maeneo yao ya kiutawala.

## 12 Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Serikali Sura ya 437

Tozo ya miamala ya simu sasa kuwa shillingi elfu nne za kitanzania(4,000) tofauti na awali ambapo ilikuwa shillingi elfu kumi( 10,000)

## 13 Sheria ya Bandari Sura ya 166

Ushuru wa bandari kukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA) na baadae makusanyo hayo kulipwa kwenye mfuko wa bandari na mlipaji mkuu wa serikali tofauti na awali ambapo ushuru wa bandari ulikuwa ukikusanywa na bandari yenyewe.

## 14 Sheria ya Uwekezaji Sura ya 38

Mamlaka ya Waziri mwenye dhamana ya fedha kutoa msamahama wa kodi kwa baadhi ya vivutio vya kikodi sasa kuidhinishwa na kamati ya Taifa ya uwekezaji, kutolewa chini ya sheria husika za kodi

15

# Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 ( The Tax Administration Act)

- Watanzania wote wenye sifa ya kupata vitambulisho vya Taifa au waliokwisha pata vitambulisho vya Taifa watasajiliwa na kamishina wa kodi na kupewa namba ya mlipakodi( TIN) chini ya Sheria ya Usajili na Utambuzi wa Watu

- Kwa walipa kodi wanaofanya kazi Zanzibar watatumia namba za mlipa kodi zilizosajiliwa na bodi ya mapato Zanzibar(ZRB)

- Tafsiri ya neno machine ya kutoa risiti za kielektoniki sasa kujumuisha risiti zinazotolewa kupitia mifumo mbalimbali ya kielektroniki au simu za mikononi.

- Washauri wote wa kodi nchini( tax consultants) watafanya kazi za ushauri wa kodi kwa niaba ya mlipa kodi au mteja kama tu watakuwa na leseni ya kufanya hivyo baada ya kutolewa na kamishina wa kodi nchini, kwa lugha nyingine hakuna mshauri wa kodi atafanya kazi ya masuala ya kodi kwa niaba ya mteja wake bila ya kuwa na leseni iliyotolewa na kamishina

- Tofauti na waajiriwa au mameneja wa watu, hakuna mtu yeyote ambaye hajasajiliwa au hana kibali cha kufanya kazi kama mshauri wa kodi( tax consultant) hatafanya kazi yoyote ya ushauri wa kodi kwa niaba ya mlipa kodi au kufanya mawasiliano yoyote yahusuyo kodi na kamishina wa kodi kwa niaba ya mlipa kodi au kujaribu kufanya uwakilishi kwa niaba ya mlipa kodi chini ya sheria yoyote ya kodi hapa nchini.

- Mshauri wa kodi(tax consultant) mwenye leseni ya kufanya kazi hiyo anaweza kusimama kama wakala wa mlipa kodi chini ya sheria yoyote ya kodi kwa mujibu ya masharti yatakayokuwa yametolewa kwenye kibali na kamishina wa kodi.

- Kamishina wa kodi nchini atahakikisha kwamba namba ya mlipakodi itakayotolewa( TIN) itaunganishwa moja kwa moja kwenye mfumo wa mamlaka ya vitambulisho vya Taifa(NIDA)

- Takwa la watanzania wenye vitambulisho vya Taifa kusajiliwa na kupewa namba ya mlipa kodi litaanza kufanya kazi rasmi tarehe 1 ya mwezi januari 2023

- Sasa ni takwa la lazima kwa kila mlipa kodi kuwasilisha ritani zake za mwaka kwa njia ya kielektroniki kabla ya tarehe iliyoaninishwa katika sheria ya kodi husika kufikia ukomo tofauti na awali ambapo takwa hili halikuwa la lazima.

# 15 Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura ya 438 ( The Tax Administration Act)

Waziri wa fedha atatunga kanuni au kuweka utaratibu wa namna gani ritani hizo zitawasilishwa kwa njia ya kielektroniki.

Kamishina wa kodi, kama atakavyoona inafaa au katika mazingira ambayo hayaepukiki anaweza kumuruhusa mlipa kodi au mtu kuwasilisha ritani zake kwa mkono.

Sasa ni takwa la lazima kwa wamiliki wote wenye maghala yenye lengo la kutunzaa bidhaa au vifaa kwa ajili ya biashara kusajili maghala hayo kwa kamishina wa kodi.

Wamiliki wote wa maghala watakaosajiliwa kwa mujibu wa sheria hii watakuwa na wajibu wa kutunza kumbukumbu zote za bidhaa au vifaa vilivyomo ndani ya ghala husika na kuwasilisha taarifa ya kila mwezi kwa kamishina kwa utaratibu ambao utaainishwa na kamishina mwenyewe.

Kama kamishina atabaini au kugundua kama kuna bidhaa au vifaa zimetunzwa kwenye ghala ambalo halijasajiliwa au mmiliki wa ghala husika amesajili lakini hakutoa taarifa ya mwezi kama sheria inavyotaka, mmiliki wa ghala husika atapigwa penati ya pointi 300 au kuwajibika kulipa hasara ya mapato ambayo atakuwa amesababisha kwa kushindwa kutoa kwake taarifa ya uwepo wa ghala hilo au bidhaa hizo bila kujali kama ghala hilo linamilikiwa na yeye au la.

Mtu yeyote mwenye sifa za kusajiliwa kama mlipa kodi au mwenye wajibu wa kuomba leseni chini ya sheria za kodi akashindwa kufanya hivyo, au akafanya nje yam da kama itakavyokuwa imeanishwa na kamishina atakuwa anatenda kosa la jinai na atapigwa faini ya shillingi 500 pointi au kifungwa cha jela kisichozidi mwaka mmoja au vyote kwa Pamoja.

Mtu yeyote mwenye sifa au wajibu wa kulipa kodi ya ushuru wa bidhaa na akashindwa kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, au akazalisha bidhaa chini ya sheria ya ushuru wa bidhaa bila leseni, au kushindwa kufuata masharti yalitolewa ndani ya leseni au akavunja utaratibu aliowekewa ndani ya leseni, au kushindwa kutii amri halali ya kutengua, kusimamisha au kufuta leseni chini ya sheria ya ushuru wa bidhaa na kamishina au au masharti mengine yoyote, kushindwa kutunza kumbukumbu za uzalishaji, kuhifadhi, kusafirisha au kuingiza bidhaa zenye sifa ya kutozwa ushuru wa bidhaa kwenye eneo lake la kazi au kiwanda, kufanya mauzo bila ya kuwa na kibali, kushindwa kutangaza kabla ya kuanza kwa uzalishaji wa bidhaa zenye sifaa ya kutozwa ushuru wa bidhaa kutoka kwenye kila jingo, chumba, eneo, machine, vifaa, atakuwa anafanya kosa la jinai na atatozwa point 330 au kwenda jela miaka isiyozidi mitatu(3) au vyote kwa Pamoja, lakini pia mahakama inaweza kutoa amri ya kutaifisha bidhaa hizo.

## 16 Sheria ya Rufaa za Kodi sura ya 408

Sasa migogoro ya kodi kutatuliwa kati ya TRA na mlipakodi( armicable settlement) bila kuhusisha msuluhishi wa kati(mediator). Mabadiliko haya yataidia kupunguza gharama kwa pande zote mbili

## 17 Sheria ya Udhamini Sura ya 318

Tafsiri ya neno mmiliki mnufaika sasa kuendana na ile iliyotolewa kwenye sheria ya Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu Sura ya 423

Mdhamini amabae hatatoa taarifa juu ya mabadiliko hayo atakuwa ametenda kosa la jinai na atapigwa faini isiyopungua shillingi laki mbili na isiyozidi millini moja.

Wadhamini sasa kuwa na jukumu, ndani ya mwezi mmoja la kumtaarifu Kabidhi Wasii Mkuu( The Administrator General) juu ya mabadiliko yoyote katika taarifa za wamiliki wanufaika ikiwemo kukoma kwa mdhamini, kuingia kwa mdhamini mpya au mabadiliko ya taariza za mdhamini.

## 18 Sheria ya Utalii Sura ya 65

Vibali vyote vya utalii sasa kutolewa na Mkurugenzi Mkuu baada ya kupata idhini ya bodi ya utalii.

# 19 Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148

Waziri mwenye dhamana ya fedha, baada ya kupata ridhaa ya baraza la mawaziri kuwa na mamlaka ya kusamehe kodi ya ongezeko la thamani kwa wawekezaji mahiri maalum baada ya kuidhinishwa na kamati ya Taifa ya uwekezaji.

# 20 Sheria ya Wakala wa Meli Sura ya 415

Shirika la meli kuwa na mamlaka juu ya upakuaji na usambazaji(clearing and forwarding) wa bidhaa zinazohusiana na usafirishaji na uingizaji wa vilipuzi, madini, kemikali zinazotumiwa na makampuni ya madini, meno ya tembo chini ya sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori.